# 10 SIRI YA SANDUKU LA DHAHABU A AGANO



Kunako nyakati za zamani, tamaduni mbali mbali, kama vile za Wainka, Waaztek, Wamaya na Wamisri, kulikuwako na hazina ya sanaa zilizotambulika sana. Kaburi la Kimisri la Tuntakhameni lilikuwa ni maalumu, ndani yake mlipatikana kikamilifu vile vilivyokuwemo pale makaburi mengine yalipochimbuliwa.

Kitu kilichostaabisha zaidi lilikuwa ni lile hekalu ambalo Musa alilijenga kule jangwani. Kila chombo, hususani vile vilivyopatikana ndani ya lile Sanduku la Agano, vilikuwa na maana ya kina kabisa. Vile vipimo vyake, vifaa vyake, mahali pake, pamoja na yale maadhimisho yaliyofanywa ndani ya lile hekalu, hivi vyote vilikuwa na siri muhimu sana. Je, kitu hiki kina maana yo yote kwetu sisi?

## *WATU WA MUNGU WALIOKOLEWAJE KATIKA ZILE NYAKATI ZA KALE?*

1. Mwanadamu alipotenda dhambi alitengwa na Mungu, na kama isingekuwa Mungu kuingilia, alihukumiwa mauti ya milele. Tokea wakati ule na kuendelea, mwelekeo wake asilia ulikuwa ni kutenda dhambi. Alikuwa dhaifu na asiye mwadilifu. Pale Mungu alipomweka mwanadamu katika Edeni, alimwonya kwamba kama angetenda dhambi angekufa. **Je, hili lilitokea mara moja? Je, ni nani aliyekufa mahali pake? Mwanzo 3:21.**

   *Wana kondoo wawili walikufa mahali pa mwanadamu. Adamu na Hawa walipewa ________________ kama mavazi. Walikuwa ni wa badala yake, ishara ya Mwokozi ajaye.*

2. **Je, ni lini ambapo Mungu aliandaa njia ya manusura ili kumwokoa mwanadamu? 1 Petro 1:18-20.** ____________________________________________

3. **Kulikuwa na njia gani pekee ya uombezi wa dhambi? Waebrania 9:22.**

   ____________________________________________

   *Hii ndio sababu ya kwamba sadaka yake Habili ilikubaliwa na ile ya Kaini haikukubaliwa. Mungu alimwagiza yule mtu aliyetenda dhambi alete mnyama ili afe mahali pake. Angeweka mikono yake juu ya kile kichwa cha yule mnyama na kuziungama dhambi zake, jambo lililoashiria kuhamishwa kwa dhambi zake kwenda kwa mhanga asiye na hatia.*

## *MUNGU AJIFUNUA MWENYEWE KWA MWANADAMU*

4. **Mungu aliwatoa Isaraeli kutoka Misri Naye akawaongoza hata nchi ya ahadi kwa namna ya kustaajabisha. Akayafunua mapenzi Yake pamoja na sheria Yake kwao. Je, Mungu katika maono alimwaagiza Musa atengeneze nini? Kutoka 25:8, 40.**

   ____________________________________________

5. **Je, vipimo vya ukumbi uliolizunguka hekalu vilikuwa ni vipi? Kutoka 27:9-19.**

   *Ulikuwa na vipimo vifuatavyo: urefu: futi 150 (dhiraa 100) juu ya nguzo ishirini; upana: futi 75 (dhiraa 50) juu ya nguzo 10 za shaba; kimo: futi 7.5. Mtu asingeweza kuchungulia.*

6. **Hekalu hili lilikuwaje?**

   *Hekalu hili, kwa kulingana na Kutoka 26, lilikuwa na vipimo, futi 40.5 urefu wake, upana futi 9, na kimo futi 7.5. Lilitengenezwa kwa mbao ya mti wa mshita zilizofunikwa kwa dhahabu. Ule mti na dhahabu viliashiria muunganiko wa asili ya kibinadamu na ya kiungu ya Kristo. Mti ulimwakilisha Kristo kama mwanadamu. Dhahabu ilimwakilisha Kristo kama Mungu.*

*Lilifunikwa kwa tabaka nne tofauti.*

- Sehemu yake ya nje ilikuwa ni ya ngozi ya pomboo ya kahawia na nyeusi na mwonekano wake haukuwa wa kuvutia sana. Iliwakilisha asili ya Kristo ya kibinadamu.
- Chini ya tabaka hili kulikuwako na ngozi nyingine ya kondoo dume mwekundu iliyowakilisha mateso ya Kristo.
- Tabaka la tatu lilikuwa la manyoya meupe ya mbuzi, yakiwakilisha usafi wa Kristo.
- Ndani, chini ya matabaka haya matatu, kulikuwako na kifuniko cha kitani nyeupe iliyodariziwa kwa rangi ya samawi, zambarau na nyekundu; rangi za kifalme zikimwakilisha Kristo kama Mfalme.

**Lile hekalu liligawanywa sehemu mbili: Mahali Patakatifu na Patakatifu Mno.**

## *VIPENGEE SABA KWA AJILI YA WAKATI WETU*

**7. Lango la ule ukumbi lilikuwa na upana wa futi 27 pamoja na pazia la kitani nyeupe nzuri lililodariziwa kwa rangi ya samawi, zambarau na nyekundu zikining'inia kutoka katika nguzo nne (Kutoka 27:16). Inamwakilisha nani? Yohana 10:9.**

a) Njia pekee ili kwenda kwa Baba. Waefeso 2:18; 1 Timotheo 2:5.


b) Je, ni kwa nini lango hili lilikuwa ni pana sana? Inaonesha upendo wa Mungu na matamanio Yake ya kumwokoa mwanadamu. 1 Timotheo 2:3, 4.

c) **Nguzo nne.** Kristo amejifunua Mwenyewe katika injili hizi nne. Wito Wake unahubiriwa katika pembe nne za dunia.

**8. Madhabahu ya kafara ilikuwa ni kielelezo cha Kalvari (Kutoka 27:1-8). Je, Yohana Mbatizaji alimwitaje Mwokozi? Yohana 1:29.** ________________________________

a) Kafara. Mnyama wa kuchinjwa alipasa kuwa mkamilifu asiye na ila. Aliiwakilisha tabia ya Kristo isiyo na dhambi. 1 Petro 1:9; Waebrania 4:15. Pale mwenye dhambi alipoweka mikono yake juu ya kichwa cha yule mnyama, alizihamisha zile dhambi zake kwenda kwa yule mnyama asiye na hatia, ambaye alikufa mahali pake. Kuna njia moja pekee ya kuepuka yale mauti ya milele, nayo ni kujipatia aliye wa badala afe mahali petu, kafara. Kristo Ndiye alikuwa kafara asiye na hatia aliyekufa pale Kalvari.

b) Zile pembe zilikuwa ni ishara ya nguvu. Ziliwakilisha nguvu ya kafara ya Kristo.



**9. Lile birika la shaba: Kutoka 30:17-21 kunatajwa kutakaswa kwa njia ya maji. Je, tufanyeje ili kuzisafisha dhambi zetu? Matendo 22:16. ______________________________**

*Je, ni nani aliye maji ya uzima? Yohana 4:14.* ______________________________________

**10. Kile kinara cha taa chenye matawi saba kilipondwa kutoka katika kipande cha dhahabu (Kutoka 25:31-39). Je, nuru hii inamwakilisha nani? Yohana 8:12.**

______________________________________________________________________

a) Mungu hutuangazia sisi nuru kwa njia ya neno Lake. Zaburi 119:105.

b) Yale mafuta huwakilisha Roho Mtakatifu. Zekaria 4:1-6.

c) Kristo anapoishi ndani yetu kwa njia ya Roho Mtakatifu, sisi tutakuwa ni nuru ya ulimwengu. Mathayo 5:14 -16.

d) Matawi saba yanaliwakilisha kanisa ambalo kwa njia yake Kristo anauangazia ulimwengu nuru. Ufunuo 1:20.

**11. Je, ile meza ya mikate ya wonyesho inamwakilisha nani (Kuotoka 25:24-30)? Yohana 6:15.**

______________________________________________________________________

a) Je, Yesu anatutaka tufanye nini ili kwamba ale pamoja nasi? Ufunuo 3:20. Tunapasa kufungua ______________________________ wa moyo wetu.

b) Anataka kutuboresha sisi kwa njia ya neno Lake na kutusaidia kukua kiroho. Mathayo 4:4.

**12. Ile madhabahu ya kufukiza (Kutoka 30:1-10) inawakilisha nini? Zaburi 141:2; Ufunuo 8:3.**

______________________________________________________________________

a) Ni kwa njia ya Yesu pekee ndipo maombi yetu yaweza kumfikia Baba na kuwa kama manukato ya kuvutia. 1 Yohana 2:1.

b) Uvumba ulifukizwa kila asubuhi na jioni, ukiwakilisha ibada ya asubuhi na jioni.



**13. Kulikuwa na nini nyuma ya pazia katika Patakatifu Mno? Waebrania 9:2-5; Kutoka 25:10-22.**

__________________________________________________________________

a) Sanduku la agano liliashiria kiti cha enzi cha Mungu. Ufunuo 11:19.

b) Zile mbao za Amri Kumi, zilizoandikwa kwa chanda cha Mungu, zilikuwamo ndani ya lile Sanduku (Kumbukumbu 10:1-5). Ndizo msingi wa kiti cha enzi cha Mungu na mng'ao wa tabia Yake (Zaburi 89:14; 119:172).

c) Kifuniko, kilichofanyizwa kwa dhahabu safi, kiliitwa ni kiti cha rehema.

d) Kilikuwa na makerubi wawili wenye mbawa zilizoinuliwa kuonyesha malaika wanaokizunguka kiti cha enzi cha Mungu.

## *HITIMISHO*

**14. Vyombo katika lile hekalu huonyesha mpango wa Mungu kwa ajili ya wokovu wa mwanadamu. Twawezaje kukua karibu zaidi na Yesu? Waebrania 4:16.**

__________________________________________________________________

a) Vitu saba vilivyotajwa hapo juu huonekana katika umbo la msalaba.

b) Vinatukumbusha sisi juu ya:

1) Lango: Kristo anatuita sisi.
2) Madhabahu: Kristo alikufa mahali petu.
3) Bakuli: Kristo anataka kututakasa sisi kutokana na dhambi zote.
4) Kinara cha taa: Kristo anataka kuyaangazia maisha yetu kwa njia ya Roho Mtakatifu.
5) Meza ya mikate ya wonyesho: Kristo anataka kutulea sisi kwa uwepo Wake na kuwasiliana nasi kwa njia ya Neno Lake.
6) Madhabahu ya kufukiza: Kristo huyawalisilisha maombi yetu kwa Baba.
7) Sanduku la agano: Linawakilisha kiti cha enzi cha Mungu. Linatuonyesha sisi ya kwamba rehema na sheria Yake ndio misingi ya serikali Yake. Yesu ndio kiini cha Maandiko, aliyeoneshwa katika vivuli vya Agano la Kale, na katika maisha Yake hapa duniani katika Agani Jipya.

---

***Uamuzi wangu:*** *Ninaamini ya kwamba Yesu Kristo ndiye kiini cha Maandiko na ya kwamba kila kielelezo katika lile hekalu ni mwendelezo ujao wa injili* ○ *Ndio* ○ *Hapana*

---